



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

# News Bulletin



[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)



Wizara ya Nishati



wizara\_ya\_nishati\_tanzania



@Nishati2017



Wizara ya Nishati

Toleo Namba 18

Septemba 1-30, 2020

## KALEMANI AIPA RUNGU TANESCO KUWAKATIA UMEME WADAIWA SUGU



UK.  
2

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akitoa hamasa kwa wananchi wa Kitongoji cha Lasawana, kijiji cha Lokili, Kata ya Kashashi, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, waige mfano wa Mzee Abrahamu Kileo (mwenye kofia ya njano), kwa kulipungu shilingi 27,000 tu ili waunganishiwe umeme. Waziri aliwasha rasmi umeme katika nyumba ya Mzee huyo akiwa katika ziara ya kazi, Agosti 17, 2020.

UK.  
5

## MGALU ATOA AGIZO ZITO KWA WAKANDARASI WA REA



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma

# KALEMANI AIPA RUNGU TANESCO KUWAKATIA UMEME WADAIWA SUGU

Veronica Simba –  
Kilimanjaro

**W**aziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuanza kuwakatia umeme wateja wake wenye madeni sugu nchi nzima, ifikapo Agosti 31, mwaka huu.

Alitoa maelekezo hayo akiwa katika ziara ya kazi wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, Agosti 17, 2020 kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme ambapo pia aliwasha umeme katika taasisi za umma na makazi ya wananchi.

Alisema TANESCO inadai zaidi ya shilingi bilioni 300 kutoka kwa Mashirika hasa ya Umma, Halmashauri, Sekta ya Afya, Mambo ya Ndani, Maji, Ulinzi na nyingine nyingi.

"Natoa siku 14 kuanzia sasa kwa Taasisi zote zinazodaiwa zikiwemo za Umma, zilipe, zisipolipa tutakata umeme, tena



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (katikati), akimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, aliyekuwa akimweleza dhamira ya ziara yake mkoani humo, Agosti 17, 2020.

bila huruma wala taarifa nyingine yoyote. Taarifa ndiyo hii," alisisitiza.

Akielezea sababu za kufikia uamuzi huo, Waziri Kalemani alisema Shirika hilo linajiendesha

kibashara pasipo kupata ruzuku serikalini, hivyo malimbikizo ya madeni ya wateja yanahatarisha uhai wake.

Ailezea baadhi ya miradi inayoendelea

kutekelezwa na Shirika hilo kwa kutumia fedha za ndani kuwa ni pamoja na

**INAENDELEA UK.**

**2**



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na wanafunzi, walimu na wakazi jirani wa Shule ya Sekondari Esinyari iliyoko Kata ya Olkolili, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, baada ya kuwashaa rasmi umeme katika Shule hiyo, Agosti 17, 2020.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto) na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadiidifu, Mhandisi Innocent Luoga, wakipita kukagua miundombinu ya umeme katika kijiji cha Ngumbili, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, Agosti 17, 2020.



## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
Mhandisi Zena Said  
(Katibu Mkuu)

**Makamu Mwenyekiti**  
Mhandisi Leonard Masanja  
(Naibu Katibu Mkuu)

**Mhariri**  
**Veronica Simba**  
(Kaimu Mkuu wa Kitengo  
cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**  
**Veronica Simba**  
**Teresia Mhagama**  
**Zuena Msuya**  
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**  
**Lucas Gordon**

Wasiliana nasi kwa simu  
namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano  
Mtumba Dodoma, S.L.P.  
2494, Dodoma

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)

## MAONI/KATUNI

# ILIPENI TANESCO IHUDUMIE WANANCHI

**H**ivi karibuni, Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwa ziarani mkoani Kilimanjaro, alitoa maelekezo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuanza kuwakatia umeme wateja wake wenye madeni sugu nchi nzima.

Waziri alitoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa wote zikiwemo taasisi za umma, taasisi binafsi na hata wafanyabiashara kulipa madeni hayo kabla hatua ya kuwakatia umeme hajiatekelezwa. Muda huo umefikia hatima Agosti 31, 2020.

Katika maelezo yake, Waziri amesema wazi kuwa amelazimika kufikia uamuzi huo ili kuinusuru TANESCO ambayo inajientesha kibiashara pasipo kutegemea ruzuku kutoka serikalini, ili iweze kuendelea kutimiza majukumu yake ya kuwashudumia Watanzania.

Takwimu zinaonesha hadi sasa Shirika hilo linadai zaidi ya shilingi bilioni 300 kutoka kwa wateja wake. Hiki ni kiasi kikubwa sana cha pesa ambacho kisipolipwa kwa wakati, Shirika litayumba kihuduma.

Wahenga walisema dawa ya deni ni kulipa. Lakini pia, kwa mtu mwenye moyo wa uzalendo kwa nchi yake, hawesi kukubali kuona TANESCO ikifilisika na kushindwa

kutoa huduma kwa wananchi. Mzalendo wa kweli atalipa deni, tena bila kunung'unika.

Sote tu mashuhuda wa huduma nzuri ambazo zimekuwa zikitolewa na Shirika hili. Umeme umefika kila kona ya nchi, tena hadi vijiji ambako nchi nydingi za kiafrika zimeshindwa kupiga hatua ambayo sisi tumefikia.

Kwa hali hiyo, tunawasihi wadaiwa wote sugu mjifakari na kuchukua hatua stahiki za kulipa madeni yenu ili kazi nzuri inayoendelea kufanya na TANESCO iendelee. Kutokulipa madeni yenu ni kuwakomoa Watanzania wanaotegemea huduma ya Shirika hili katika kuendesha shughuli zao za kiuchumi na hata kijamii.

Tumuunge mkono Jemedari wetu, Rais John Pombe Magufuli anayefanya kila awezalo kuhakikisha nchi yetu inapaa kiuchumi. Kutokulipa kile tunachodaiwa na TANESCO ni kurudisha nyuma jithada za Rais wetu maana hakuna uchumi wa viwanda pasipo umeme.

Haya shime wadau wetu, tafadhali lipeni madeni yenu pasipo kusubiri huduma ya umeme ikatwe katika taasisi zenu kisha muanze kunung'unika. Ilipeni TANESCO iendelee kuwashudumia wananchi.

## Katunika Ki-nishati



# KALEMANI AIPA RUNGU TANESCO KUWAKATIA UMEME WADAIWA SUGU



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwapa uhakika akina mama wa kijiji cha Ngumbili, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, kuwa umeme utakuwa umewashwa katika eneo hilo kabla ya Septemba 15, 2020. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme, Agosti 17, 2020.

**INAENDELEA UK.**

**10**

ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gridi ya Taifa mkoani Kigoma pamoja na kusambaza miundombinu mingine katika vijiji na mitaa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

"Kwahiyio ni lazima tuwe na vyanzo vya uhakika vya ndani ambavyo pamoja na mambo

mengine, ni kwa wateja wetu kutulipa kwa wakati."

Aidha, Dkt Kalemani alitahadharisha kuwa wakati wa utekelezaji wa suala hilo, asipigiwe simu na wadaiwa zenyen mlengo wa kumsihi kusitisha wataalamu na sababu ambayo hutolewa na wengi kuwa taasisi zao ni muhimu hivyo zisikatiwe umeme. Alisitiza kuwa badala ya kupiga simu, wadaiwa

walipe ankara zao.

Katika hatua nyingine, akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, Waziri alimweleza kuwa Mkoa huo una umeme mwangi ikilinganishwa na mahitaji yake.

Alisema kuwa Mkoa una zaidi ya megawati 110 za umeme wakati matumizi yake ni megawati 45 hadi 48, hali inayoufanya kuwa na ziada kubwa kuliko mahitaji.

Aidha, alieleza kuwa kwa sasa Serikali kupitia Wizara yake, inafuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji inayoendelea, ambayo ni REA II na REA III.

Alisema ameunda kikosi kazi maalumu kinachojumuisha wataalamu kutoka wizarani, TANESCO Makao Makuu na REA Makao Makuu, kitakachowajibika kuhakikisha Miradi hiyo ya umeme inakamilika ifikapo Septemba 15, 2020.

Kwa upande wake,

Mkuu wa Mkoa alipongeza kazi kubwa inayofanywa na Wizara lakini akaomba kusimikwa kwa nguzo za umeme zilizo imara zaidi, hususan katika maeneo ya milima ambako kuna upepo mkali, ili ziweze kuhimili hali hiyo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema Wilaya yake ina deni kwa Rais John Magufuli ambalo inawiwa kulilipa kutokana na kuwajali wananchi hao kwa kuendelea kuwapigania katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo umeme.

Katika ziara hiyo, Waziri alifuatana na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadiifu, Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Dkt Tito Mwinuka, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga pamoja na Wataalamu wengine mbalimbali kutoka Wizarani na katika Taasisi hizo.



Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu (kushoto), akimwombwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, kufikisha salamu za pongezi na shukrani kwa Rais John Magufuli, kutoka kwa wananchi wa Wilaya hiyo kutokana na jitihada zake kuwapelekea maendeleo ikiwemo umeme. Waziri aliwasha rasmi umeme katika Kitongoji cha Lasawana, kijiji cha Lokili, Kata ya Kashashi, wilayani humo akiwa katika ziara ya kazi, Agosti 17, 2020.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt Tito Mwinuka (kulia) na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga, wakiwa katika ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), Kata ya Olkolili, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, Agosti 17, 2020.

# MGALU ATOA AGIZO ZITO KWA WAKANDARASI WA REA



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Namonge, Kata ya Namonge, Wilaya ya Bukombe, Mkoani Geita, kabla ya kuwashaa umeme kwenye kijiji hicho, Agosti 17, 2020.

## Hafsa Omar - Geita

**N**aibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amesema Serikali haitapokea Mradi wowote kutoka kwa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi ya Umeme Vijijini (REA)

mpaka pale itakapofanya ukaguzi na kujiridhisha kuwa masharti yote ya mkataba yamezingatiwa.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti, Agosti 17, 2020, akiwa wilayani Chato na Bukombe, mkoani Geita, kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi za usambazaji

umeme vijijini.

Aidha, alitoa tahadhari kwa Wakandarasi wa Mradi wa REA III Mzunguko wa Kwanza,



Wananchi na wanafunzi wa Shule ya Msingi Itanga iliyopo katika Kijiji cha Itanga, Kata ya Minkoto, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza nao akiwa kwenye ziara ya kukagua kazi ya usambazaji umeme vijijini, Agosti 17, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mhandisi Charles Kabeho (kulia), wakielekea kukata utepe na kuwashaa rasmii umeme katika Shule ya Msingi Itanga iliyopo katika Kijiji cha Itanga, Kata ya Minkoto, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, Agosti 17, 2020.

unaotarajiwa kukamilika Septemba 15 mwaka huu, wakae tayari kwa ukaguzi na uhakiki kabla ya kukabidhi Mradi huo.

"Wakandarasi wote wa miradi ya REA tutawakagua tuone ni namna gani walivyofanya kazi zao, kwamba ni kweli idadi ya kilomita walizopewa zote wamezifanyia kazi. Tutakagua idadi ya wateja, transforma na kila kitu kama mkataba unavyosema," alisema Mgalu.

Naibu Waziri alitoa wito kwa wakandarasi hao kutoondoka katika maeneo ya kazi mpaka pale makabidhiano yatakapofanyika kwa mujibu wa taratibu za kisheria zilizowekwa.

Alieleza kuwa, Wizara ya Nishati inajivuria mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Rais John Magufuli, ambapo mpaka sasa takribani taasisi za umma 15,000 zimeunganishwa na

INAENDELEA UK.

6

# MGALU ATOA AGIZO ZITO KWA WAKANDARASI WA REA



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo, akiwasha umeme katika Shule ya Msingi Itanga iliyopo katika kijiji cha Itanga, Kata ya Minkoto, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, Agosti 17, 2020.

**INAENDELEA UK.**

**5**

umeme.

Akieleza zaidi, alisema

kuwa, Serikali baada ya kuona imefanikiwa katika jithihad za kupeleka umeme vijijini, kwasasa imeamua kuelekeza nguvu za kupeleka umeme kwenye

vitongoji ambapo zaidi ya shilingi bilioni 800 zimetengwa kwa ajili ya

kazi ya usambazaji umeme kwenye vitongoji.

Pia, aliwashukuru viongozi wa Wilaya na Mkoa kwa kumsimamia kikamilifu Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa REA mkoani humo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba, alisema kuwa atahakikisha anamsimamia kikamilifu Mkandarasi wa Mkoa huo, ili aweze kumaliza kufanya kazi zake kwa mujibu wa muda aliopewa na Serikali.

Vilevile, alisema amefurahiswa na dhamira ya Serikali ya kuhakikisha umeme unafika katika taasisi mbalimbali za umma akisema nishati hiyo itasaidia kuboresha huduma zinazotolewa katika taasisi hizo.

Naibu Waziri pia aliwasha umeme katika Shule ya Msingi Itanga iliyopo katika Kijiji cha Itanga, Kata ya Minkoto, Wilaya ya Chato na katika Shule ya Sekondari ya Namonge, Kata ya Namonge Wilaya ya Bukombe, na alikagua njia ya kusafirishia umeme katika kijiji cha Kazibizyo, Wilaya ya Bukombe, Mkoani Geita.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo, (wa tatu-kulia) akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika Shule ya Sekondari ya Namonge, Kata ya Namonge, Wilaya ya Bukombe, mkoani Geita, Agosti 17, 2020. Wa nne kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (mwenye ushungi) na Mkuu wa Wilaya ya Bukombe Said Nkumba (mwenye kofia) wakimsikiliza Mhandisi Bakar Abdallah (wa kwanza-kulia), walipokuwa kwenye ukaguzi wa njia ya kusafirishia umeme katika kijiji cha Kazibizyo, Wilaya ya Bukombe, mkoani Geita, Agosti 17, 2020.

## BILIONI 100 KUPELEKA UMEME PEMBEZONI MWA MIJI

**Veronica Simba –  
Arusha**

S erikali imetenga shilingi bilioni 103.8 kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa majiji, mikoa, manispaa na miji, nchi nzima.

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, alibainisha hayo kwa nyakati tofauti, Agosti 16, 2020 alipokuwa katika ziara ya kazi wilayani Arusha.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kuwashaa umeme katika Shule ya Sekondari Moivaro na baadaye Shule ya



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akisisitiza jambo kwa wataalamu aliofuatana nao katika ziara yake kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme, wilayani Arusha, Agosti 16, 2020. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt Tito Mwinuka na kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga. Wa pili kutoka kushoto ni Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga.

Sekondari Nyahiri Terrat, Dkt Kalemani alisema kuwa Serikali inaendelea kuwaunganishiwa umeme wananchi wa maeneo ya aina hiyo nchini kote kwa gharama ya shilingi 27,000 tu kama ilivyo kwa vijijini.

Alisema, Mpango huo wa Serikali ni kutokana

na uhalisia kuwa maeneo hayo kwa kiasi kikubwa, yanashabihiana na yaliyoko vijijini, ambapo asilimia kubwa ya wakazi wake wana kipato kidogo.

“Tulikaa tukaona maeneo haya yaliachwa muda mrefu bila kuwa na miundombinu ya umeme.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwahamasisha wananchi wa Mtaa wa Bondeni Kati, Kata ya Terrat, wilayani Arusha, kulipia shilingi 27,000 tu ili waunganishiwe umeme. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi wilayani Arusha, kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme, Agosti 16, 2020.

Tukaona tuwapunguzie gharama kutoka mlivyokuwa mnalipa zamaani shilingi 177,000 na katika baadhi ya maeneo 380,000 hadi shilingi 27,000 tu.”

Akizungumzia Wilaya ya Arusha, Waziri Kalemani alisema kuna mitaa takribani 26 iliyopembезони mwa Mji na kwamba Serikali ilianza kuipeleka umeme kutoka mwaka 2018.

Alimpungeza Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Arusha, Mhandisi Herin Muhina, kwa kazi nzuri anayoifanya na kumwagiza atumie muda wa miezi mitatu kuanzia hivi sasa, kukamilisha kazi ya kupeleka umeme katika mitaa yote iliyopembезони mwa Mji, ambayo haijafikiwa na huduma hiyo.

Aidha, Waziri alikiri kufurahishwa na Uongozi wa Shule ya Sekondari Moivaro kuona umuhimu wa kulipia gharama za kuunganishiwa umeme na kupata huduma hiyo, ikiwa na mwaka mmoja tu tangi ianzishwe.

Alitoa rai kwa viongozi wengine katika maeneo mbalimbali nchini, kuiga mfano huo kwa kuhakikisha taasisi zote za umma zinapewa kipaumbele katika kuunganishiwa umeme ili kuongeza tija katika utoaji huduma kwa wananchi.

Kuhusu suala la wananchi kulipia nguzo ili waunganishiwe umeme, Dkt Kalemani aliendelea kusitiza msimamo wa Serikali kuwa ni marufuku kwa kitendo hicho na alitoa tahadhari kwa yejote atakayebainika kwenda kinyume na maagizo hayo, atachukuliwa hatua kali. Alisitisiza wananchi

**INAENDELEA UK.**

## BILIONI 100 KUPELEKA UMEME PEMBEZONI MWA MIJI

INAENDELEA UK.

10

kuendelea kulia huduma ya umeme pasipo kusubiri nguzo akisema hilo siyo jukumu lao. "Wewe lipia kisha udai umeme," amesitiza.

Katika hatua nyingine, Waziri aligawa vifaa vya Umeme Tayari (UMETA) kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Arusha, ikiwa ni ishara ya kuthamini mchango wao kwa Taifa kupitia kazi wanayoifanya katika kuhabarisha na kuelimisha jamii juu ya masuala mbalimbali, yakiwemo ya



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akikata utepe kabla ya kuwashaa rasmi umeme katika Shule ya Sekondari Moivaro, wilayani Arusha, Agosti 16, 2020. Wa pili kutoka kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi.

sekte ya nishati.

Aidha, aligawa vifaa hivyo kwa shule alizoziwashia umeme pamoja na walimu wake huku akielekeza kuwa

vitumike kuwaunganishia umeme wa gharama nafuu ambao haulazimu kutandaza mfumo wa nyaya katika jengo husika. Kwa upande wake,

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi, alimponeza Waziri Kalemani kwa uchapakazi wake hususan katika kuhabarisha wananchi wa maeneo mbalimbali nchini kote, wanapata huduma ya umeme.

"Uchapakazi wako unadhihirisha kwa vitendo kuwa unamuunga mkono Rais wetu mpewa, Mheshimiwa John Magufuli katika kuwatumikia Watanzania ili kuhakikisha wanajipatia maendeleo ya kiuchumi."

Katika ziara hiyo, Waziri aliambatana na viongozi mbalimbali akiwemo Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadiidifu, Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt Tito Mwinuka, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na wataalamu wengine mbalimbali kutoka wizarani na taasisi hizo.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akiwakabidhi Waandishi wa Habari, Mkoa wa Arusha, vifaa vya Umeme Tayari (UMETA), ili waunganishiwe katika nyumba zao. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua miradi mbalimbali ya umeme wilayani Arusha, Agosti 16, 2020.

# HABARI PICHANI



Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi akizungumza, wakati wa hafla fupi ya kuwasha umeme katika Shule ya Sekondari Nyahiri Terrat. Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia-Meza Kuu) ndiye aliwasha rasmi umeme katika Shule hiyo akiwa katika ziara ya kazi, Agosti 16, 2020.



Mwonekano wa Jengo lenye baadhi ya vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Nyahiri Terrat, wilayani Arusha, baada ya kuwashisha rasmi umeme na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwa katika ziara ya kazi, Agosti 16, 2020.

Sehemu ya umati wa wananchi wa Kata ya Terrat, wilayani Arusha, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), alipokuwa akizungumza nao, muda mfupi kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Shule ya Sekondari Nyahiri Terrat, Agosti 16, 2020.



Baadhi ya Wafanyakazi wa TANESCO wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), alipokuwa akizungumza katika hafla ya kuwasha rasmi umeme katika Shule ya Sekondari Nyahiri Terrat, wilayani Arusha, Agosti 16, 2020.



# WAZIRI KALEMANI AAGIZA MKANDARASI AFUTIWE MKATABA

**Veronica Simba – Arusha**

**W**aziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani ameagiza kufutwa Mkataba wa kazi wa Mkandarasi, kampuni ya M/s Nipo Group Limited, aliyekuwa akitekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza mkoani Arusha, kutokana na utendaji usioridhisha.

Alitoa maagizo hayo Agosti 15, 2020 kwa Uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), akiwa katika ziara ya kazi kijijini Lendikinya, Kata ya Sepeko, wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha.


Dkt Kalemani alilazimika kutoa maelekezo hayo baada ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa kazi husika katika maeneo kadhaa ya Wilaya hiyo, ambapo alibaini kuwa Mkandarasi husika



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Lendikinya, Kata ya Sepeko, wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha (hawapo pichani), alipokuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, Agosti 15, 2020.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani), akikagua moja ya nguzo zilizosimikwa kwa muda mrefu na Mkandarasi M/s Nipo Group Limited, pasipo kuvutiwa nyaya za umeme ili kuwaunganishia wananchi wa kijiji cha Lendikinya, wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha, akiwa katika ziara ya kazi Agosti 15, 2020. Waziri ameagiza Mkataba wa Mkandarasi huyo ufutwe.



Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Edward Balele, akitoa salamu za kumkaribisha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (Mwenye miwani - Meza Kuu), ili azungumze na wananchi. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, kijiji cha Lendikinya, wilayani Monduli, Agosti 15, 2020.

ametelekeza kazi hiyo kwa muda mrefu, akiacha nguzo zilizosimikwa pasipo kuvuta nyaya wala kuunganisha umeme.

Akizungumza na wananchi wa Lendikinya, Waziri aliwaelea kuwa Mkandarasi husika alianza kazi hiyo tangu mwaka 2018 na alipaswa akamilishe mwishoni mwa mwezi huu, lakini utekelezaji wake unasusua ambapo ana miezi zaidi ya mitatu hajaonekana kazini.

Sambamba na kufuta Mkataba, Waziri pia alielekeza Mkandarasi huyo akatwe asilimia 10 ya malipo yake kutokana na kuchelewesha kazi.

Akiendelea kutoa maelekezo, Waziri aliwataka TANESCO na REA kumpatia kazi hiyo Mkandarasi mwingine mwenye uwezo au ifanywe na TANESCO wenyewe na kuhakikisha inakamilika ifikapo mwishoni mwa

**INAENDELEA UK.**

**11**

# WAZIRI KALEMANI AAGIZA MKANDARASI AFUTIWE MKATABA



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), akiwatambulisha kwa wananchi baadhi ya viongozi aliofuatana nao katika ziara yake kijiji cha Lendikinya, wilayani Monduli, Agosti 15, 2020. Kutoka kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt Tito Mwinuka na Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga.

INATOKA UK.

10

mwezi Septemba, mwaka huu.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa hatua zote zifuate utaratibu wa manunuzi, kisheria na kimkataba.

Katika hatua nyingine Waziri aliagiza kukamatwa na Polisi, kuwekwa ndani na kuhojiwa Mwakilishi wa Mkandarasi huyo aliyekuwepo katika ziara ya Waziri ili atoe maelezo kuhusu pesa ambayo Serikali imelipa kwa kazi

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwatanza akina mama wa kijiji cha Lendikinya, wilayani Monduli, waliokuwa wakimlaki kwa nyimbo alipowasili kijijini hapo Agosti 15, 2020 akiwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

husika, imetumika vipi.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Edward Balele kutumia Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata Wakurugenzi wa Kampuni husika ambao hawakushiriki katika ziara hiyo, ili wahojiwe walikopeleka pesa ya Serikali.

“Naagiza wasakwe wale Wakurugenzi wenyewe, maana huyu aliyepo ni mfanyakazi tu, wapatikane na wahojiwe ili watusaidie pesa walizolipwa zimekwenda wapi. Hizi ni pesa za Watanzania.”

Awali, akimkaribisha Waziri kuzungumza na wananchi, Mkuu wa Wilaya alimponeza Dkt Kalemani kwa ufuatiliaji makini wa kazi ambao umemwezesha kubaini udhaifu wa Mkandarasi husika na kuchukua hatua stahiki zinazolenga kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya umeme kama Serikali ilivyodhamiria.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt Tito Mwinuka na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga, waliunga mkono maamuzi ya Waziri na kumwahidi kuwa watatekeleza maagizo yote aliyoyatoa.

Kwa mujibu wa taarifa ya TANESCO Mkoa wa Arusha, iliyowasilishwa kwa Waziri, Mkataba wa Mkandarasi husika ni wa miezi 24 ambao ulianza Machi 2018.

Mkandarasi amefikia asilimia 65 ya kazi husika ambapo kwa mujibu wa Mkataba, alipaswa kuwa amefikia asilimia 92 hadi sasa kwa malengo ya kukamilika Agosti 30, mwaka huu.

Mradi unatarajiwa kusambaza umeme katika vijiji 126 kwa Mkoa mzima na kuunganishia umeme wateja wapatao 5,428.



Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazaji Umeme na Huduma kwa Wateja kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Makao Makuu, Mhandisi Raymond Seya (kushoto) na Msimamizi wa Miradi ya Umeme Vijijini, Kanda ya Kaskazini kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Shukurani Rugaimukamu, wakiwa katika Mkuano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na wananchi wa kijiji cha Lendikinya, Wilaya ya Monduli (hawapo pichani), Agosti 15, 2020.

# SERIKALI YAITAKA KAMPUNI YA ANDOYA KUONGEZA UZALISHAJI UMEME

Zuena Msuya - Ruvuma

**N**aibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, ameitaka kampuni ya Andoya inayozalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi kutanua wigo wa kampuni hiyo ili kuongeza uzalishaji zaidi.

Masanja alisema hayo Agosti 01, 2020, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma, wakati wa ziara yake ya kutembelea mradi huo ili kuona maendeleo yake.

Kampuni ya Andoya huzalisha umeme ambao huliuzia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na pia katika vijiji vitatu vilivyo jirani ambavyo ni Lifakara, Kilimani na Mbangamao.

Masanja aliueleza Uongozi wa Andoya kuwa wana uwezo na nafasi kubwa ya kuweza kutanua mradi huo na kuongeza uzalishaji wa umeme kwakuwa eneo la mradi ni kubwa na linatosha.

"Kampuni yenu ina nafasi kubwa ya kukua



kiuzalishaji kwa sababu mna chanzo cha uhakika ambacho kina maji ya kutosha na yanayopatikana muda wote. Azma ya serikali ni kuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 10,000 za umeme ifikapo mwaka 2025. Hivyo, mchango wa wazalishaji wadogo unahitajika sana," alisema Mhandisi Masanja.

Aidha, alizitaka taasisi za kifedha kuendelea kushirikiana na kuwaunga mkono wazalishaji binafsi wa umeme nchini kwa kuwapatia mikopo pale inapohitajika kwa lengo la kujenga, kuboresha au kutanua wigo wa mradi husika kwakuwa miradi hiyo inadumu kwa muda mrefu.

Aliwataka wasimamizi wa mradi huo waendelee kuusimamia vizuri ili uendelee kuzalisha umeme huku akibainisha kuwa miradi ya kuzalisha umeme wa maji, ikisimamiwa vizuri, hudumu kwa muda

**INAENDELEA UK.**

**13**



Meneja wa kituo cha kuzalisha umeme cha Andoya, Jasper Bubelwa, akitoa maelezo ya uzalishaji wa umeme unaofanywa na kampuni hiyo kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa pili-kulia), alipofanya ziara Agosti 1, 2020, kukagua kituo hicho kinachozalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi uliopo Mbinga mkoani Ruvuma.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akikagua mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi, kazi inayofanywa na kampuni ya Andoya, alipofanya ziara Mbinga, mkoani Ruvuma, Agosti 01, 2020.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, (katikati), akitoa maagizo kwa Meneja wa kituo cha kuzalisha umeme cha Andoya, Mhandisi Jasper Bubelwa, alipofanya ziara ya kukagua shughuli za kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi, wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, Agosti 01, 2020.

# SERIKALI YAITAKA KAMPUNI YA ANDOYA KUONGEZA UZALISHAJI UMEME

INATOKA UK.

12

mrefu.

Vilevile, aliaagiza wasimamizi wa mradi huo kubadilisha mita za umeme zinazotumiwa na wateja wao katika vijiji vitatu vilivyo karibu na mradi huo ambazo ni za mfumo wa kizamani zinazomruhusu mteja kutumia kwanza huduma ya umeme ndipo alipie. Badala yake, aliwataka wawafungie mita za LUKU zinazotumika sasa ambazo mteja hulipia umeme kadri anavyotumia.

Aliendelea kusisitiza kuwa jukumu la serikali kupitia Wizara ya Nishati ni kutunga Sera na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika sekta ya nishati. Kwa muktadha huo, Wizara pamoja na Taasisi zake itaendelea kusimamia sheria, taratibu na kanuni za uwekezaji katika sekta husika ili kuendelea kuvutia wawekezaji nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kampuni husika, Alex Andoya aliishukuru Wizara ya



Nishati na Taasisi zilizo chini yake, kwa ushirikiano walioutoa kwa kampuni hiyo tangu kuanzhishwa kwake hadi sasa.

Aidha, aliahidi kushirikiana na taasisi za kifedha kuongeza uzalishaji wa umeme katika mradi huo kama alivyoshauriwa.

Akieleza kwa ufupi kuhusu mradi huo, alisema kuwa ujenzi wake

ulibuniwa na Marehemu Baba yake Mzee Mbunda Andoya na ulijengwa kwa awamu mbili, ya kwanza ikiwa ni ujenzi wa mtambo wa kuzalisha megawati 0.5 ambapo ujenzi ulianza mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2015.

Alisema, awamu ya pili ilihuisha uwekaji wa mtambo wa megawati 0.5 ambapo ulikamilika mwaka

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia), akipata maelezo katika eneo la bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Andoya, Alex Andoya (kushoto), alipofanya ziara ya kukagua shughuli za kuzalisha umeme katika kampuni hiyo, Mbinga, mkoani Ruvuma, Agosti 01, 2020. Wa pili kutoka kushoto ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga na wa pili kutoka kulia ni Mkurugenzi Mwanzilishi wa Kampuni hiyo, Janeth Andoya.

2018 na kuwa na jumla ya mitambo yenyewe kuzalisha wa megawati moja.

Katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu aliambata na Ujumbe kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).



Aina ya mita zinazotumiwa na wateja wa umeme unaozalishwa na kampuni ya Andoya. Kampuni hiyo huzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi uliopo Mbinga, mkoani Ruvuma. Mita hizo humruhusu mteja kutumia umeme kabla ya kulipia.



# MATUKIO PICHANI

14



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, akiwasili katika eneo la bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi, alipofanya ziara ya kukagua shughuli za kuzalisha umeme zinazofanywa na Kampuni ya Andoya, wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, Agosti 01, 2020.



Eneo la bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, kukagua shughuli za kuzalisha umeme zinazofanywa na kampuni ya Ndoya, wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, Agosti 01, 2020.



Jiwe la Msingi la Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi, wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, alikagua Mradi huo unaoteklezwa na kampuni binafsi ya Andoya, Agosti 01, 2020.



Moja ya nguzo zinazotumika kusambaza umeme unaozalishwa na Kampuni ya Andoya kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Mtandazi, wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma.



**Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (wa kwanza-kushoto) akiwasili kwenye Kituo cha Afya Bukiriro, kilichopo Kata ya Bukiriro, Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera, Agosti 16, 2020. Katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Michael Mntenje na kulia ni Mganga Mkuu wa Kituo hicho, Dkt Wilbroad Bukiriro. Naibu Waziri aliwasha rasmi umeme kituoni hapo.**



**Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo, akitata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika Shule ya Sekondari Nyakahuru, iliyopo katika Kijiji cha Mabale, Kata ya Nyakahura, Wilaya ya Biharamulo, Agosti 16, 2020.**

## KASI YA USAMBAZAJI UMEME KATIKA TAASISI ZA UMMA YAONGEZAKA

Hafsa Omar - Kagera

**N**aibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo, amesema Serikali itaendelea kuzipa kipaumbele taasisi za umma nchini katika usambazaji wa umeme vijijini ili ziweze kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Aliyasema hayo kwa nyakati tofauti, Agosti 16, 2020 akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua miradi ya usambazaji umeme vijijini katika Wilaya za Ngara na Biharamulo, mkoani Kagera.

Akiwa mkoani humo, Naibu Waziri aliwasha umeme katika Vituo vya Afya Bukiriro wilayani Ngara na Nyakahuru wilayani Biharamulo. Aidha, aliwasha umeme katika Shule kadhaa za Sekondari.

Alisema kuwa, sekta ya nishati ina nafasi kubwa kuziwezesha sekta nyingine zifanikiwe kwakuwa bila ya umeme, sekta ya afya itashindwa kutoa huduma bora kwa watanzania



**Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akifurahia jambo alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Muyenzi kilichopo Kata ya Rulenge, Wilaya ya Ngara, Mkoani Kagera, alipokuwa kwenye ziara kukagua kazi ya usambazaji umeme vijijini, Agosti 16, 2020.**

kwani huduma nyingi na muhimu kwenye vituo vya afya zinategemea nishati ya umeme.

Aliongeza kuwa, kwasasa Serikali inajenga vituo vingi vya afya nchini na kwa kuzingatia hilo, sekta ya nishati imeamua kuongeza kasi zaidi ya usambazaji umeme katika vituo vya afya ili Watanzania wapate huduma bora.

Kwa upande wa elimu, Naibu Waziri alisema kiwango cha ufaulu nchini kimeongezeka hasa katika maeneo ya vijiji kwasababu ya kazi nzuri ya usambazaji umeme vijijini ambapo shule nyingi ambazo zipo kwenye vijiji hivyo zimeunganishwa na umeme.

Alisema kuwa, umeme umeboresha sekta ya elimu nchini na kuwataka wanafunzi kutumia umeme huo kikamilifu kwa ajili ya kujisomea na kujiongezea ufaulu katika shule zao.

Aidha, alimtaka mkandarasi wa mkoaa huo kuendelea kusambaza umeme katika maeneo ambayo yamesalia kwakuwa mradi huo upo ukingoni na wananchi

## KASI YA USAMBAZAJI UMEME KATIKA TAASISI ZA UMMA YAONGEZeka

INATOKA UK.

15

wa vijiji hivyo wanahitaji huduma hiyo.

Pia, aliwatoa hofu wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa kuwahakikishia kupatikana kwa umeme wa uhakika mara baada ya kumalizika kwa miradi mikubwa ya umeme.

"Serikali inatekeleza miradi mikubwa miwili ya umeme inayojenga njia ya kusafirisha umeme na vituo vyake, mradi mmoja ni Bulyanhuru - Geita wenyenjia ya kusafirisha ya msongo wa kilovoti 220 na mwingine ni Geita - Nyakanazi wa msongo wa kilovoti 220. Yote inatarajiwaa kukamilika mwakani na itakuwa ndiyo



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Muyenzi iliyopo Kijiji cha Muyenzi, Kata ya Rulenge, Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera wakimshangilia Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (hayupo pichani) alipowasili katika Shule hiyo kuwashaa rasmi umeme, Agosti 16, 2020.



Wananchi wa kijiji cha Bukiriro, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza nao akiwa kwenye ziara ya kazi kukaguwa miradi ya usambazaji umeme vijiji, Agosti 16, 2020.

mwarobaini wa tatizo la kukatika umeme,"alisema.

Alilipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa juhudi zake mbalimbali kwa kutatua changamoto za umeme zinazojitokeza mkoani humo.

Naye Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha Bukiriro, Dkt Wilbroad Bukiriro, aliihukuru Serikali kwa kupeleka umeme kwenye kijiji hicho na kuwezesha kituo hicho kupata umeme baada ya kutokuwa na nishati hiyo tangu kilipoanzishwa mwaka 1977.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri pia aliwasha umeme katika Shule ya Sekondari ya Muyenzi iliyopo kijiji cha Muyenzi, Kata ya Rulenge, Wilaya ya Ngara na Shule ya Sekondari Nyakahura, Kata ya Nyakahura.

# WAZIRI AAGIZA MKANDARASI WA REA AKATWE MSHAHARA



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani-kushoto), akimwagiza Meneja wa TANESCO Mkao wa Dodoma, Mhandisi Frank Chambua (kulia), kuhakikisha anamsimamia Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza, mkoani Dodoma, Kampuni ya A2Z Infra Engineering Limited, kusimika nguzo zote zilizorundikwa chini na kuwaunganishia wananchi umeme. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, wilayani Chemba, Agosti 12, 2020.

**Veronica Simba –  
Dodoma**

**W**aziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani,


ameagiza Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, mkoani Dodoma akatwe asilimia 10 ya malipo yake kutokana na

kuchelewa kukamilisha kazi hiyo.

Alitoa maagizo hayo, Agosti 12, 2020 baada ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huo katika maeneo mbalimbali



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, Simon Odunga (wa pili-kushoto) akizungumza jambo, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili-kulia) wilayani humo, kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, Agosti 12, 2020.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), akitoa maeleko kwa Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, mkoani Dodoma, Kampuni ya A2Z Infra Engineering Limited (kushoto) kuhakikisha wanakamilisha kazi hiyo kabla ya Septemba 15, mwaka huu, alipokuwa katika ziara ya kazi wilayani Chemba, Agosti 12, 2020. Kulia kwa Waziri ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Simon Odunga.

ya Wilaya ya Chemba.

Akiwa amefuatana na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, Waziri Kalemani aliutaka Uongozi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kukata kiasi hicho cha malipo ya Mkandarasi husika, ambaye ni Kampuni ya A2Z Infra Engineering Limited, kuanzia Juni 30, 2020 muda ambao alipaswa kukamilisha Mradi.

Sambamba na agizo hilo, Waziri pia alimtaka Mkandarasi huyo kukamilisha kazi ya kuunganisha umeme katika vijiji vyote 66 vilivybakia kabla ya Septemba 15 mwaka huu, huku akisisitiza kuwa, hakutakuwa na nyongeza ya muda wala msamaha.

“Asipomaliza ndani ya wakati huo, mchukulieni hatua za kisheria na kimkataba. Maeneo yatakayobaki, fanyeni ninyi TANESCO kwa pesa hiyo.”

Katika kuhakikisha kazi hiyo inatekelezwa, Waziri alimwelekeza Mkuu wa Wilaya kushikilia hati za kusafiria za Wakandarasi husika na kuhakikisha hawatoki nje

**INAENDELEA UK.**

**18**



Meneja wa TANESCO Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Frank Chambua (wa nne - kulia), akimweleza jambo Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa tatu - kulia), wakati wa ziara ya Waziri wilayani Chemba, kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji, Agosti 12, 2020. Wa pili kutoka kulia ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Simon Odunga.

Baadhi ya Vibarua wa Mkandarasi anayetekeliza Mradi wa Umeme Vijiji, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, mkoani Dodoma, Kampuni ya A2Z Infra Engineering Limited, wakiendelea na kazi hiyo jirani na kijiji cha Kwa Mtoro, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), wilayani Chemba, Agosti 12, 2020.

# WAZIRI AAGIZA MKANDARASI WA REA AKATWE MSHAHARA

INATOKA UK.

17

ya Mkoa wa Dodoma, hadi watakapokamilisha kazi hiyo.

Aidha, alimwagiza Mkandarasi huyo kuungeza vibarua na magenge, ili aweze kukamilisha kazi kwa wakati.

Vilevile, alimtaka kuondoa mara moja nguzo zote zilizorundikwa chini na kuzisimika, kuvvuta nyaya na kuwaunganishia umeme wananchi.

"Kiu ya wananchi ni kuona umeme unawaka katika nyumba zao. Hawependezewi kuona nguzo zikiwa zimerundikana chini, nanyi mkipitapita pasipo kuwashashia umeme," alisisitiza Waziri.

Dkt Kalemani alitoa wito kwa Wakandarasi wote nchini, wanaoendelea kutekeleza Miradi ya REA III, kuhakikisha wanakamilisha ifikapo



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, wakiwa katika ziara kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji, wilayani Chemba, Mkoa wa Dodoma, Agosti 12, 2020.

Septemba 15, 2020.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya alimshukuru Waziri kwa kufuatilia utekelezaji wa Mradi husika huku akiweka wazi kuwa hana imani na Mkandarasi huyo kutokana na kutotekeliza majukumu

yake ipasavyo.

Aliahidi kufanya kazi maelekezo yote ya Waziri katika kumsimamia Mkandarasi ili kuhakikisha anakamilisha kazi hiyo na hivyo wananchi wapate huduma ya umeme kama ilivyokusudiwa na Serikali. Katika Taarifa yake

kwa Waziri, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Frank Chambua alieleza kuwa, kati ya vijiji 581 vya Mkoa huo, vijiji 393 vimeshapata umeme ambavyo ni sawa na asilimia 67.47 ya vijiji vyote.

# NAIBU WAZIRI WA NISHATI AWATAKA WAKANDARASI KUFANYA KAZI KWA WELEDI



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kufika katika kijiji cha Ilula, Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, Agosti 15, 2020.

## Hafsa Omar - Mwanza

**N**aibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo amewataka wakandarasi wanaofanya kazi za

usambazaji umeme vijijini kufanya kazi kwa weledi, uaminifu na kwa kasi ili kuweza kufanikisha kazi zao kwa wakati.

Aliyasema hayo Agosti 15, 2020 wakati

akizungumza na wananchi wa kijiji cha Busolwa, Kata ya Igokelo, Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akizungumza na wananchi (hawapo pichani) wa Kijiji cha Ilula, Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, kabla ya kuwashwa umeme kwenye kijiji hicho Agosti 15, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (wa pili - kulia), akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika Shule ya Sekondari Imalilo, Iliyopo katika kijiji cha Kibitilwa, Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, Agosti 15, 2020.

umeme vijijini.

Aidha, alisema Serikali haitasita kusitisha mkataba wa mkandarasi yeyote nchini ambaye hataendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano.

"Nataka nitoe wito kwa wakandarasi kufanya kazi kwa bidii kwa sababu Wananchi wanahitaji huduma ya umeme, na bila hivyo, itasababisha kushindwa kumaliza kazi kwa wakati katika maeneo yao," alisema.

Alisema Serikali imeamua kutoa nafasi kwa wakandarasi wazawa kufanya kazi ya usambazaji umeme ili kuwawezesha wananchi wake waweeze kujajiri na kujiimarisha katika kazi zao.

"Tangu tumeingia kwenye Wizara hii, ni zaidi ya mara 10 tumekuwa tukifanya vikao mbalimbali na wakandarasi mjini Dodoma, tukifanya tathmini na kutoa maagizo mbalimbali ili kuona namna bora ya kuweza kuwasaidia wakandarasi hao kufanya kazi kwa weledi," alisema Mgalo.

Pia, alisema Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lina wataalamu

**INAENDELEA UK.**

**20**

INATOKA UK.

19

wa kutosha na wenyewe uwezo wa kufanya kazi ambazo zinafanywa na wakandarasi wengine, lakini Serikali iliamua kutoa nafasi kwa wakandarasi binafsi, nafasi ambayo baadhi ya wakandarasi wameshindwa kuitumia vizuri.

Aliipongeza Kampuni ya ETDCO ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO, inayoendeleza kazi ya usambazaji umeme vijijini Mkoani Mwanza, akisema imefanya kazi nzuri.

"Nimekuja kukagua kazi inayofanywa na Mkandarasi ambaye amechukua nafasi ya Mkandarasi Nipo Group. Nimeona ETDCO inafanya kazi nzuri sana," alisema.

Naibu Waziri, alimtaka Mkandarasi huyo kufanya kazi hiyo kwa haraka zaidi kwakuwa wananchi wa vijiji hivyo wamesubiri huduma ya umeme kwa muda mrefu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Juma Sweda aliiomba Serikali iendelee kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ya

## NAIBU WAZIRI WA NISHATI AWATAKA WAKANDARASI KUFANYA KAZI KWA WELEDI



Wananchi wa Kijiji cha Busolwa, Kata ya Igokelo, Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (hayupo pichani), wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi za usambazaji umeme vijijini, Agosti 15, 2020.

Wilaya hiyo, hasa katika migodi ambako wananchi wengi wamejajiri.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri aliwasha umeme katika Zahanati ya Kijiji cha

Ilula na Shule ya Imalilo, Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (mwenye ushungu) akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa kampuni ya ETDCO, katika Kijiji cha Busolwa, Kata ya Igokelo, Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, wakati wa ziara yake kukagua kazi za usambazaji umeme vijijini, Agosti 15, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Imalilo, iliyopo katika Kijiji cha Kibitilwa, Kata ya Ilula, Wilaya ya Kwimba, akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi za usambazaji umeme vijijini, Agosti 15, 2020.

# MRADI WA PERI URBAN KUKAMILIKA KWA WAKATI

**Hafsa Omar - Dodoma**

**N**aibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, amewataka Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa miji (Peri-Urban) kukamilisha utekelezaji wa miradi yao ndani ya muda uliopangwa.

Aliyasema hayo Agosti 19, 2020, alipokuwa kwenye kikao na Wakandarasi hao, Ofisi za Wizara ya Nishati, jijini Dodoma.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga, Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangila, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt Tito Mwinuka na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga.

Akizungumza katika kikao hicho, Mhandisi Masanja alisema Mradi huo unatarajiwa kukamilika Septemba 15, mwaka huu na kusisitiza kuwa Wakandarasi hao hawataongezewa muda kwakuwa Serikali ilio muda wa kutosha kutekeleza Mradi husika.

Aliungeza kwamba, Wakandarasi wote walikubaliana na Serikali kuwa watafuata masharti yote ya mikataba waliyosaini hivyo akawataka kufuata miongozo yote ya mikataba hiyo ili kukamilisha kazi husika.

"Miradi hii ya Peri-Urban inatekelezwa sehemu ambazo watu

wana uhitaji mkubwa wa umeme; ni sehemu ambazo shughuli za kiuchumi zipo nyingi, watu wanahitaji maendeleo, bila ya umeme shughuli za kiuchumi zitakwama, kwahiyo tujitahidi kumaliza miradi hii kwa wakati," alisema.

Aidha, aliwataka Wakandarasi hao kufanya kazi kwa uzalendo kwakuwa Serikali iliamua kuwapa kipaumbele wao kama wazawa na kutochukua wanaotoka nje ya nchi, kwa kuzingatia kuwa kampuni zilizopo nchini zina uwezo wa kufanya kazi hizo.

Alifafanu kuwa, Serikali imeamua kuweka mikakati ya makusudi ili kuwajengea wananchi wake uwezo, ndio maana ikaamua kwenye miradi husika.

Naibu Katibu Mkuu alieza vigezo ambavyo vitumika katika kuwapata Wakandarasi wa miradi mingine ya umeme, kuwa ni pamoa na utendaji kazi mzuri kwenye miradi iliyopita hivyo akawataka kufanya kazi kwa weledi ili



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, akizungumza katika kikao baina ya Serikali na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa miji (Peri-Urban), kilichofanyika, Agosti 19, 2020, jijini Dodoma.

waweze kupata kazi hizo.

Wakandarasi waliohudhuria kikao hicho kutoka Kampuni za Sinotec Co. Ltd, Ceylex Engineering Ltd, Sengerema, Namis Corporate Ltd na Derm Electrics Ltd, walisaini makubaliano ya kumaliza kazi ya miradi hiyo kwa muda uliopangwa.

Kwa upande wake, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu,

Edward Ishengoma, alisema Serikali itawasimamia wakandarasi hao ili kuakikisha wanafanya kazi kikamilifu na kumaliza ndani ya muda uliopangwa.

Naye Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga, aliwataka wakandarasi hao kuelekeza nguvu zao zote katika kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na kufanya kazi kwa bidii.



Kutoka kushoto ni Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga na Kamishna Msaidizi Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangila wakiwa katika kikao baina ya Serikali na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa miji (Peri-Urban), kilichofanyika Agosti 19, 2020, jijini Dodoma.

# MATUKIO PICHANI

22



Wakandarasi wanaotekeleza  
Mradi wa Umerne katika maeneo  
yaliyo pembezoni mwa miji  
(Peri-Urban), wakiwa katika  
kikao na Naibu Katibu Mkuu  
wa Wizara ya Nishati, Mhandisi  
Leonard Masanja, Agosti 19,  
2020 jijini Dodoma.

1



2



3

**PICHA 1,2 na 3**

Wakandarasi wanaotekeleza  
Mradi wa umeme katika maeneo  
yaliyo pembezoni mwa miji  
(Peri-Urban) kutoka Kampuni  
za Sinotec Co. Ltd, Ceylex  
Engineering Ltd, Sengerema,  
Namis Corporate Ltd na  
Derm Electrics Ltd, wakisaini  
makubaliano kati yao na Serikali  
kuwa watakamilisha kazi  
husika kwa wakati. Walisaini  
makubaliano hayo Agosti 19,  
2020 jijini Dodoma.

# WANANCHI WAHAMASISHWE KUTUMIA UMEME - MGALU



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili katika Kijiji cha Mazae, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, Agosti 13, 2020.

**Hafsa Omar - Dodoma**

**N**aibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo amewataka viongozi wa Serikali za Mitaa kuwahamasisha wananchi wanaoishi katika maeneo yao, kutumia umeme kwa kulipia huduma hiyo ili waweze kuunganishiwa.

Aliyasema hayo, Agosti 13, 2020 wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi

wa kazi ya usambazaji umeme vijijini katika Kijiji na Kata ya Mazae, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma kabla ya kuwasho umeme katika Shule ya Msingi ya Mazae kijijini humo.

Alisema kuwa hajaridhishwa na kasi ya uunganishwaji wa umeme katika kijiji hicho na kuwataka viongozi kufanya mikutano ya kuwahamasisha wananchi wa maeneo yao



Wananchi wa Kijiji cha Mazae, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (hayupo pichani) wakati akiwa kwenye ziara ya kazi ya ukaguzi wa usambazaji umeme vijijini, Agosti 13, 2020.

kulipia huduma ya umeme ili wananchi wafaidike na huduma hiyo kwani Serikali inatumia gharama kubwa kufanikisha jambo hilo.

Naibu Waziri aliyataja baadhi ya maeneo ambayo huduma ya umeme imefika lakini wananchi wake bado hawajalipia huduma hiyo kuwa ni pamoja na Isomvu, Chungu, Darajani, Nyabu na maeneo mengine katika kijiji hicho.

"Serikali imepunguza gharama ya kuunganisha umeme vijijini ambayo ni shilingi 27,000 tu. Mradi huu unakaribia kufika ukingoni lakini wananchi wanaonekana hawajalipia na Mkandarasi amesema kuwa wakilipa yuko tayari kuwaunganishia. Hivyo niwaombe wananchi milio kwenye

**INAENDELEA UK.**

**24**



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mazae, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, wakati akiwa kwenye ziara ya kazi ya kukagua usambazaji umeme vijijini Agosti 13, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (mwenye kilemba) akiwa mwenye furaha, mara baada ya kukata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika Kijiji cha Mazae, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, Agosti 13, 2020.

# WANANCHI WAHAMASISHWE KUTUMIA UMEME - MGALU



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (mwenye kilemba) akiwa pamoja na Walimu na Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mazae iliyopo wilayani Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma, mara baada ya kuwasha umeme katika Shule hiyo, Agosti 13, 2020.

INATOKA UK.

23

wigo katika maeneo ambayo mradi umefika mlipie ili muunganishiwe umeme,"alisitisita.

Aliwaeleza wananchi wa kijiji hicho kuwa, Serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma ya umeme na tayari imeingia katika utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu

ya Tatu, Mzunguko wa Pili (REA III - 2) pamoja na Mradi wa Ujazilizi.

Aidha, alisema kazi ya usambazaji umeme nchini inapimwa kwa wananchi wengi kupata huduma hiyo ili wateja wengi wapatikane na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lioneze wateja na mapato na liweze kuijendesha wenyewe.

Alisema kuwa zaidi ya bilioni 800 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya usambazaji umeme ambapo kuanzia Agosti 20 mpaka

Septemba 20, mwaka huu, Serikali itakuwa inakabidhi kazi ya usambazaji umeme kwenye vijiji na vitongoji nchini kwa wakandarasi wapya.

Aidha, aliwataka wananchi ambao vijiji na vitongoji vyao bado havijafikiwa na miradi ya umeme kutokuwa na hofu kwani maeneo yao yatafikiwa na miradi hiyo hivi karibuni. Aliongeza kuwa, tayari Serikali imepeleka umeme kwenye vijiji takribani 9,512 nchini.

Naye, Hamis Israel,

mkazi wa kijiji hicho, aliishukuru Serikali kwa kuwapelekea huduma ya umeme na kuiomba kushughulikia changamoto wanazozipata wananchi wakati wakiomba kupatiwa huduma hiyo.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri pia alikagua kazi ya usambazaji umeme katika Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro na kuwasha umeme katika kijiji cha Lumuma na baadaye kugagua umeme katika makazi na maeneo ya biashara.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (mwenye kilemba) akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Morogoro wakati wa ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali ya Kijiji na Kata ya Lumuma, Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Agosti 13, 2020.

# SERIKALI YAUNDA TIMU MAALUM KUMSIMAMIA MKANDARASI WA REA KILIMANJARO

**Veronica Simba –  
Kilimanjaro**

**W**aziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani ameunda Timu maalumu inayojumuisha wataalamu mbalimbali wa Serikali ili kumsimamia Mkandarasi anayetekeleza miradi ya umeme vijiji, Mkoa wa Kilimanjaro.

Alitangaza uamuhi huo katika mukutano wa hadhara na wananchi wa Kitongoji cha Kambi ya Nyuki, wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, Agosti 17, 2020 muda mfupi kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Chuo cha Ualimu Mong'are.

Kuundwa kwa Timu hiyo itakayoongozwa na Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga kunatokana na kusuasua kwa Mkandarasi husika, Kampuni ya Urban

& Rural Engineering Services Ltd katika kutekeleza kazi zake.

"Timu hii maalumu ya watu sita, itafanya kazi kwa muda wa siku 14 kuanzia leo ili kuhakikisha

Mkandarasi anakamilisha kazi kwa wakati, ifikapo Septemba 15 mwaka huu," alifanua Waziri.

Waziri alimwagiza Mkandarasi husika kuweka Magenje matano

ya kazi katika Wilaya ya Hai ili kuharakisha kazi husika. Aidha, aliwataka Wakurugenzi wa Kampuni hiyo kuungana na Wafanyakazi wao ili kuongeza nguvu na msukumo wa kazi.

Alikemea tabia ya Wakurugenzi hao kutokufika katika maeneo ya kazi na kuwaachia wafanyakazi wao pekee ambao hata hivyo Serikali imebaini hawalipwi mishahara yao kwa wakati hivyo kuchangia kuzorota kwa kazi.

Vilevile, alitoa maelekezo kwa Wakandarasi husika kutokuondoka Hai hadi watakapokamilisha kazi hiyo.

"Ninaagiza Wakandarasi hawa wakiwemo Wakurugenzi wao, wote wasiondoke hapa Hai hadi



Baadhi ya Vibarua wa Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijiji wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro wakiendelea na kazi katika Kitongoji cha Kambi ya Nyuki, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani wilayani humo, Agosti 17, 2020.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto) akintambulisha Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga kwa wananchi wa Kitongoji cha Kambi ya Nyuki wilayani Hai, Agosti 17, 2020. Waziri alimteua Mhandisi Luoga kuongoza Timu maalumu itakayomsimamia Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijiji mkoani Kilimanjaro ili akamilishe kazi kwa wakati.



Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Sabaya akizungumza wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) wilayani humo, Agosti 17, 2020.

# SERIKALI YAUNDA TIMU MAALUM KUMSIMAMIA MKANDARASI WA REA KILIMANJARO

INATOKA UK.

25

watakapokamilisha kazi. Aidha, ninaagiza wawe wanaripoti kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Hai, kila siku saa tatu asubuhi ili tujiridhishe kuwa wapo kazini. Mkuu wa Wilaya, tusaidie kusimamia hilo," alisisitiza Waziri.

Maelekezo mengine aliyotoa Waziri ni kwa Wakandarasi kuhakikisha vibarua wote wanavaa nguo maalumu za kazi na kuwa na vifaa vyote vinavyowalinda na madhara zikiwemo kofia ngumu, buti na soksi za mikono.

Aidha, alielekeza wafanyakazi na vibarua wote walipwe ujira wao kwa wakati huku akisisitiza kuwa Mkandarasi atakayebainika kutotekeleza maagizo hayo, atachukuliwa hatua kali za kisheria na kimkataba.

Awali, akitoa salamu



Sehemu ya umati wa wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Mong'are, wilayani Hai, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani. Waziri aliwasha rasmi umeme katika Chuo hicho Agosti 17, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.

za kumkaribisha Waziri, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Sabaya alipongeza utendaji kazi mzuri wa Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wilayani humo lakini akalalamikia utendaji unaosuasua wa Mkandarasi husika.

"Mkandarasi hajafanya

kazi ya kutosha. Tulipaswa kuwa tumesimika transfoma 37 katika Wilaya yetu lakini hadi sasa amesimika transfoma saba tu."

Waziri alimtaka Mkandarasi huyo kukamilisha kazi ifikapo Septemba 15, 2020 na akaahidi yeyé mwenyewe

kwenda kuwasha rasmi umeme katika vijiji vyote vilivysalnia.

Timu iliyoundwa inajumuisha wataalamu kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO Makao Makuu na Wakala wa Nishati Vijiini (REA) Makao Makuu.



Sehemu ya umati wa wananchi wa Kitongoji cha Kambi ya Nyuki, wilayani Hai, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, alipozungumza nao kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Chuo cha Ualimu Mong'are, wilayani humo, Agosti 17, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Kambi ya Nyuki, wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, muda mfupi baada ya kuwasha rasmi umeme katika Chuo cha Ualimu Mong'are, Agosti 17, 2020. Kushoto kwa Waziri ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Sabaya.

# Naibu Katibu Mkuu Nishati akagua maendeleo ya Mradi wa JNHPP



Mafundi wakiendelea na kazi ya kukamilisha lango la handaki la kuchepusha maji ya mto wakati wa kujenga bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya bonde la Mto Rufiji, katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi huo, Agosti 22, 2020.

## Zuena Msuya - Morogoro

**N**aibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, amekagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP).

Mhandisi Masanja alifanya ukaguzi huo Agosti 22, 2020 katika eneo la bwawa la maji ili kuona maendeleo yake.

Aidha, alitembelea maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa mradi huo likiwiemo handaki la kuchepusha maji ya Mto, handaki la kupeleka maji katika mitambo ya kufua umeme, pamoja na sehemu litakapoengwa jengo maalumu la kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme.

Vilevile alikagua mitambo ya kusaga

na kuchakata kokoto pamoja na mitambo ya kuchanganya zege ambayo inatumika katika shughuli za ujenzi katika eneo la

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kushoto) akipata maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa handaki la kuchepusha maji katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), kutoka kwa Mhandisi Mkazi ambaye pia ni Mshauri wa Mradi huo, Mhandisi Mushubila Kamuhabwa (kulia). Mhandisi Masanja alikuwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi husika, Agosti 22, 2020.

## Mradi.

Kazi ya ujenzi wa mradi huo ilianza rasmi Juni 15, 2019 ambapo unatekelezwa kwa kipindi

cha miezi 36 na unatarajiwaa kukamilika Juni 2022, chini ya Mkandarasi wa ubia wa Kampuni ya Arab Contractors na El Sewedy.



Kazi ya kuandaa eneo la kujenga jengo maalum la kuendeshea mitambo, ikiendelea katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), wilayani Rufiji, Mkoa wa Pwani, wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja ya kukagua maendeleo ya ujenzi wake Agosti 22, 2020.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kushoto) akipata maelezo ya ufanyaji kazi wa mitambo ya kuchanganya zege kutoka kwa Mhandisi Mkazi na Mshauri wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Mhandisi Mushubila Kamuhabwa (kulia), wakati wa ziara yake kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi husika, Agosti 22, 2020.



Mwonekano wa mitambo ya kuchanganya zege inayotumika wakati wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi huo, Agosti 22, 2020.



Sehemu itakayowekwa Mikanda ya kusafirisha zege kutoka mitambo ya kuchanganya zege hadi kwenye bwawa la kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP). Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi huo Agosti 22, 2020.



Ujenzi wa mahandaki matatu ya kupeleka maji ya kuzungusha mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Bonde la Mto Rufiji katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), ukiendelea wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja kukagua maendeleo yake, Agosti 22, 2020.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati) akitazama shughuli za ujenzi zinazoendelea katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), alipofanya ziara ya kukagua maendeleo yake, Agosti 22, 2020. Kushoto kwake ni Mhandisi Mkazi na Mshauri wa Mradi huo, Mhandisi Mushubila Kamuhabwa.

# WAZALISHAJI UMEME BINAFSI WATAKIWA KUPUNGUZA GHARAMA



**Hafsa Omar - Dodoma**

**W**aziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, amewataka wazalishaji binafsi wa umeme nchini kuzingatia maelekezo ya Serikali ya kupunguza bei ya nishati hiyo katika maeneo ambayo wanatoa hudumu husika.

Aliyasema hayo Agosti 6, 2020, katika kikao na wazalishaji wadogo wa umeme nchini, kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, jijini Dodoma.

Katika kikao hicho, Waziri aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leornad Masanja, na viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zake.

Aliwaelea wawekezaji hao kuwa Serikali haitatua muda wa ziada wa majadiliano kuhusu jambo hilo, kwasababu imeshatoa muda wa kutosha wa kuwasikiliza; kilichobaki ni utekelezaji wa maagizo hayo.

"Tumekaa hapa pamoja ili kuona namna bora

kwenda kulitatu jambo hili. Takribani miaka 10 iliyopita tulifungua milango kwa uwekezaji na tunaendelea kufungua milango hiyo, lakini tunataka uwekezaji wenyе manufaa kwa pande zote mbili, ninyi mpate faida na wananchi pia wapate huduma yenye manufaa kwoo,"alisema.

Aliongeza kuwa, ni matarajio ya Watanzania kuona manufaa ya kazi za wawekazaji hao na kwamba Serikali itahakikisha inasimamia na kuondo kero zote ambazo zimejitokeza katika miradi hiyo.

Alieleza kuwa, bei ya kuunganisha umeme kwa wateja kwa maeneo ambayo wawekezaji hao wanatekeleza miradi husika hailingani na uhalisia wa hali ya maisha ya wananchi wa kawaida wa maeneo hayo ambapo wananchi wengi hushindwa kulpia huduma hiyo kutokana na gharama kubwa wanazotozwa.

Aidha, alisitisiza kuwa, gharama za umeme kwa wateja nchini lazima zifanane kwani nchi ni moja. "Haiwezekani nchi moja kuwe na bei tofauti za



Kutoka kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, Kamishna Msaidizi Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangila na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga wakiwa kwenye kikao baina ya Viongozi wa Wizara na wawekazaji wadogo wa umeme nchini, kilichofanyika katika Ofisi za Wizara jijini Dodoma, Agosti 6, 2020.

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (katikati), akiongoza kikao baina ya viongozi wa Wizara na wawekazaji wadogo wa umeme nchini, kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati, Dodoma, Agosti 6, 2020. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Zena Said.

huduma ya umeme. Serikali haiko tayari kuona hayo."

Alifanua kuwa, Serikali imefanya ukaguzi na kugundua kuwa kuna kero nyingi ambazo wananchi wanazipata kuhusiana na wawekezaji husika.

"Wananchi wengi wamelalamika umeme ni mdogo, hauna nguvu. Hiyo ni kero lazima tuikubali. Tunajenga uchumi wa viwanda hivyo huwezi kumpelekea umeme mwananchi wa kuwashaa taa peke yake, lazima umeme umsaide mwananchi kwa shughuli za kiuchumi," alisema.

Dkt Kalemani aliwashukuru wakezaji hao kwa ushirikiano wao na kuwataka waone umuhimu wa kushughulikia jambo hilo ambalo linawatesa wananchi.

Kwa upande wake, Mhandisi Matthew Matimbwi ambaye ni mzalishaji wa umeme alisema wamepokea kauli hiyo kwa mikono miwili na wapo tayari kushirikiana na Serikali kutatua kero hizo ambazo zinawapata wananchi.

Alisema kuwa, kwa upande wao wapo tayari kuendelea na kazi ya kuzalisha umeme ili wananchi ambao wanaishi pembezoni waendelee kupata nishati ya umeme jadidifu kwa bei ambayo Serikali imependekeza.

## MATUKIO PICHANI

30



Kutoka kushoto ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt Tito Mwinuka na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhiliti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Godfrey Chibulunje, wakiwa kwenvye kikao baina ya Viongozi wa Wizara ya Nishati na wawekazaji wadogo wa umeme nchini, kilichofanyika katika Ofisi za Wizara jijini Dodoma, Agosti 6, 2020.



3



**PICHA 1,2 na 3**  
Baadhi ya Wajumbe wakifuatilia kikao kati ya Wizara ya Nishati, Taasisi zake pamoja na wawekazaji wadogo wa umeme wa nchini. Kikao hicho kiliongozwa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, Ofisi za Wizara Dodoma, Agosti 6, 2020.

## MKANDARASI WA REA SINGIDA AAMRIWA KURIPOTI POLISI



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mbele), akikagua maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II), kijiji cha Kisiriri, wilayani Iramba, Mkoa wa Singida, Agosti 13, 2020.

### Veronica Simba – Singida

**S**erikali imewagiza Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Pili (REA II) mkoani Singida, kuripoti Polisi kila siku ili kuthibitisha kuwa yupo kazini hadi atakapokamilisha kazi hiyo.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, Agosti 13, 2020 akiwa ziarani mkoani humo kutokana na kutoridhishwa na utendaji kazi wa Mkandarasi husika, ambaye ni muunganiko wa Kampuni ya EMEC Engineering Ltd na Dynamic Engineering and System Company Ltd.

Alisema, Mradi huo umekuwa ukisuasua tangu mwaka 2018 muda ambaa ulipaswa kukamilika, kutokana na sababu za kitaalamu na kiutendaji,

hivyo Serikali imelazimika kuhakikisha unakamilika ifikapo Septemba 10, 2020.

Akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Waziri alimwelekeza Mkuu wa Mkoa, Dkt Rehema Nchimbi kumsimamia Mkandarasi huyo na kutomruhusu kutoka nje ya Mkoa huo hadi atakapokamilisha kazi. Aidha, alimwagiza kumweka chini ya ulinzi Mkandarasi endapo hatakamilisha kazi kwa wakati.

“Kuanzia kesho, viongozi na wataalamu wa Kampuni hii wawe wanarioti Polisi na kuweka saini ili kuthibitisha wapo kazini. Nami mnileetee taarifa ya kila wiki ili nione nani alisaini na yupi hakusaini, alisisitiza Waziri.

Alielekeza wasimamizi wa Mradi huo kutoka Wakala wa Nishati Vijijini



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto), akizungumza na vibarua wa Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II), mkoani Singida, alipotembelea kukagua kazi inayoendelea katika kijiji cha Kisiriri, wilayani Iramba, Agosti 13, 2020.

(REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kufuutilia maendeleo ya kazi ya Mkandarasi huyo kwa muda wa siku saba na endapo hataonesha mwelekeo wa kuikamilisha kwa wakati, wafute Mkataba wake na wao wenyewe waikamilishe.

Sambamba na kufuta Mkataba wake endapo hatakamilisha kazi, Waziri aliwaagiza TANESCO na REA kumchukulia Mkandarasi huyo hatua za

kisheria na za kimkataba.

Waziri alimtaka Mkandarasi kuongeza idadi ya vibarua na aweke magenge manne katika kila Wilaya ili kuongeza kasi ya kazi.

Awali, wakiwasilisha kwa nyakati tofauti, taarifa ya utekelezaji wa Mradi huo kwa Waziri, Mkurugenzi wa Huduma za Ufundji (REA), Mhandisi Jones Olotu na Meneja

INAENDELEA UK.

32



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kisiriri, wilayani Iramba, Mkoa wa Singida (hawapo pichani), alipokuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA II), Agosti 13, 2020.

## MKANDARASI WA REA SINGIDA AAMRIWA KURIPOTI POLISI



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dkt Rehema Nchimbi, akizungumza wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake alipofika ofisini kwake, Agosti 13, 2020 akiwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji.

**INATOKA UK.**

**31**

wa TANESCO Mkoa wa Singida, Francis Kaggi, walikiri utendaji dhaifu wa Mkandarasi huyo.

Miongoni mwa changamoto walizozieleza ni pamoja na kasi isiyoridhisha ya Mkandarasi huyo kulingana na muda wake kimkataba. Aidha, walisema kuwa, Mkandarasi amesimika nguzo kwa muda mrefu pasipo kuvuta nyaya kwa baadhi ya vijiji.

Nyingine ni kuwa na magenge mawili tu na vibarua wachache wasioweza kukidhi nguvukazi inayohitajika ili kukamilisha kazi husika kwa wakati.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa, Dkt Nchimbi aliunga mkono kuwa utendaji wa Mkandarasi hauridhishi hivyo akamshukuru Waziri kwa kufuatilia na kuwekea mkazo utekelezaji wa Mradi husika.

Aliahidi kutekeleza yale yote yaliyoelekezwa na Waziri katika kuhakikisha



Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Msafiri Baraza (kushoto) na baadhi ya Watendaji wa Kampuni ya Mkandarasi anayetekeliza Mradi wa Umeme Vijiji Awamu ya Pili (REA II) mkoani Singida, wakifuatilia kikao cha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo (hawapo pichani), Ofisini kwa Mkuu wa Mkoa, Agosti 13, 2020. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme vijiji



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na vibarua wa Mkandarasi anayetekeliza Mradi wa Umeme Vijiji Awamu ya Pili (REA II), mkoani Singida pamoja na wananchi, alipotembelea kukagua kazi inayoendelea katika kijiji cha Kisiriri, wilayani Iramba, Agosti 13, 2020.

Mkandarasi anafanya kazi yake ipasavyo.

Mkandarasi aliahidi mbele ya Waziri kukamilisha kazi hiyo kwa wakati na kutekeleza maelekezo yake yote.

Mkandarasi huyo anatekeleza kazi katika Wilaya zote za Mkoa wa Singida ambapo mpaka sasa utekelezaji wake uko chini ya asilimia 20. Mradi unatakiwa uunganishie umeme wananchi 3,000 lakini hadi sasa waliouanganishwa ni chini ya 1,000.

Katika hatua nyingine, Waziri amewaasa Watanzania waishio vijiji, ambao hawa jafikiwa na umeme

nchini kote kuwa wastahimilivu kwani Serikali itanza kusambaza wakandarasi wa kufanya kazi hiyo kuanzia Agosti 20 hadi Septemba 20, mwaka huu.

Alisema Wakandarasi hao watafanya kazi ya kusambaza umeme kwa vijiji na vitongoji vyote vili vyosalia nchini ndani ya kipindi cha miezi 12.

Katika ziara hiyo, Waziri pia alikagua kazi inayoendelea ya kupeleka umeme katika kijiji cha Kisiriri, wilayani Iramba na kumtaka Mkandarasi kuwa amewasha umeme kabla ya Septemba 10, 2020.



Mafundi na vibarua wa Mkandarasi anayetekeliza Mradi wa Umeme Vijiji Awamu ya Pili (REA II) mkoani Singida, wakiendelea na kazi katika kijiji cha Kisiriri, wilayani Iramba, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), Agosti 13, 2020.

# KIWANDA CHA KUZALISHA VIUNGANISHI VYA UMEME CHAFUNGULIWA DAR

**Veronica Simba –  
Dar es Salaam**

**W**aziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, ameweka jiwe la msingi la kiwanda cha kitakachojihusisha na utengenezaji wa vifaa vinavyotumika kuunganisha mifumo ya umeme, maarufu kwa jina la kigeni kama 'insulators'.

Aliweka jiwe hilo, Agosti 10, 2020 katika eneo la kiwanda cha Inhemeter, Kinondoni jijini Dar es Salaam, katika hafla iliyowashirikisha viongozi mbalimbali wa Serikali, wafanyakazi wa kiwanda husika na baadhi ya wananchi.

Katika hotuba yake alioitoa muda mfupi kabla ya kuweka jiwe la msingi, Dkt Kalemani alitoa pongozi kwa uongozi wa kiwanda hicho, kuitikia wito wa Serikali, uliotolewa kwa wawekezaji kuanzisha viwanda mbalimbali nchini.

Aidha, alipongeza Serikali kwa kuweka sera, dira na mwelekeo madhubuti wa kujenga uchumi wa viwanda akisema ndivyo vilivyowezesha wawekezaji mbalimbali kuendelea kuanzisha viwanda nchini.

"Hili ni tukio muhimu sana. Kwa mara ya kwanza hapa nchini, tunazindua Mradi wa aina hii. Pongezi nyingi kwa Serikali na hongereni sana uongozi wa kiwanda."

Akielezea jitihada zilizofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati, katika kuhakikisha vifaa mbalimbali vya umeme vinatengenezwa nchini na kuachana na kasumba iliyozoleka ya kuagiza kutoka nje, Dkt Kalemani alisema mkakati huo umekuwa ukitekelezwa hatua kwa hatua na umekuwa wenye mafanikio.

Alisema hatua ya kwanza ilikuwa mwaka 2017 ambapo Serikali iliweka zuijua la kuleta baadhi ya vifaa vya kuunganishia umeme kama vile nguzo, kutoka nje ya nchi.

"Leo viko viwanda 13 vya kuzalisha nguzo za umeme hapa nchini kutoka kiwanda kimoja tu kilichokuwepo awali," alieleza.

Waziri alifanua kuwa, hatua ya pili ilifanyika mwaka 2018 kwa Serikali kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuzalisha mita za umeme, ambapo alitoa shukrani kwa kampuni ya Inhemeter na Baobab, ambao walianza



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akifunua kitambaa ikiwa ni ishara raski ya kuweka jiwe la msingi katika kiwanda cha Inhemeter kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

kujenga viwanda hivyo.

Alisema, hatua iliyofuata ilikuwa ni kuweka zuijua la kuagiza nyaya za umeme kutoka nje ya nchi, ambapo kufuatia hatua hiyo, hadi sasa kuna viwanda vinne vya kuzalisha nyaya hizo hapa nchini, kutoka kiwanda kimoja cha TANALEC kilichokuwepo awali.

Akieleza zaidi, Waziri alisema baada ya hapo alitoa maelekezo kwamba ifikapo Oktoba 2020, Serikali haitaruhusu kuingiza vifaa vya viunganishi kutoka nje ya nchi badala yake vizalishwe hapa nchini.

"Nashikuru Oktoba bado haijafika. Leo ni

mwezi wa nane ambapo tunafunga kiwanda hiki cha kuzalisha viunganishi. Hongereni sana," alipongeza Waziri.

Waziri Kalemani, alitumia fursa hiyo kusisitiza msimamo wa Serikali kwamba, kuanzia sasa, hakuna ruksa kwa kifaa cha aina yoyote kinachotumika kusambaza umeme, kitakachoruhusiwa kuagizwa kutoka nje ya nchi, hususani kwa miradi inayotegemea fedha za Serikali.

Aidha, alieleza kufarrijika na taarifa aliyopewa na uongozi wa kiwanda cha Inhemeter kuwa, wanatarajia siku za usoni, kuanza uzalishaji wa nyaya maalumu zinazotumika kupitisha umeme ardhini na chini ya maji.

Waziri aliwahakikishia wawekezaji hao soko la uhakika la bidhaa zao lakini akawatahadharisha kuwa wasitumie mwanya huo kupandisha bei bali waweke bei zenye ushindani wa soko.

Katika hatua nyingine, alisema uunganishaji umeme vijiji ni umefikia vijiji 9,512 kati ya 12,257



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi wa kiwanda cha Inhemeter kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

# KIWANDA CHA KUZALISHA VIUNGANISHI VYA UMEME CHAFUNGULIWA DAR



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo (kushoto), akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi wa kiwanda cha Inhemeter kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (meza kuu-katikati), alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

INATOKA UK.

33

vilivyopo nchi nzima. Aliongeza kuwa, kuanzia tarehe 20 Agosti hadi 20 Septemba, 2020, Serikali itaanza kupeleka wakandarasi watakaofanya kazi ya kusambaza umeme katika vijiji na vitongoji vyote vilivysalisa.

"Niwtateo hofu wananchi ambao vijiji au vitongoji vyao havijafikiwa na umeme kwani wote watafikiwa kabla ya Juni 2021. Pesa za kutekeleza Mradi huo tunazo ambapo jumla yake ni takribani shilingi bilioni 851."

Awali, akizungumza wakati akimkaribisha Waziri Kalemani, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni,

Daniel Chongolo, alishukuru na kupongeza jitihada za Serikali kuitia sekta ya nishati, zilizowezesha uwekezaji katika maeneo mbalimbali, kutokana na kuwepo uhakika wa upatikanaji wa umeme.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Abrahamu Rajakili alisema kitaajiri watanzania takribani 120 na kwamba kina uwezo wa kuzalisha viunganishi milioni 1.5 kwa mwaka, huku kikilenga soko la ndani na nje ya nchi.

Kiwanda cha Inhemeter kimekuwa kikizalisha mita za umeme kabla ya kuwekeza takribani shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuanza kuzalisha viunganishi vya mifumo ya umeme.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia) na Mwakilishi wa Wawekezaji wa Kiwanda cha Inhemeter, Mustafa Rashid, wakijadiliana jambo wakati wa hafla ya ufunguzi wa kiwanda hicho kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri Kalemani alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt Tito Mwinuka (kulia) na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Amos Maganga (kushoto), wakifuatilia hafla ya ufunguzi wa kiwanda cha Inhemeter kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri wa Nishati Dkt Kalemani (hayupo pichani), alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.



Kutoka kulia ni Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidfu, Mhandisi Styden Rwebangira, Katibu wa Waziri wa Nishati, Mhandisi Robert Dulle na Afisa Nishati Mhandisi Anthony Karomba, wakifuatilia hafla ya ufunguzi wa kiwanda cha Inhemeter kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri wa Nishati Dkt Kalemani (hayupo pichani), alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati-waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi pamoja na Wafanyakazi wa Kiwanda cha Inhemeter kitakachokuwa kikizalisha viunganishi vya mifumo ya umeme. Waziri Kalemani alifungua kiwanda hicho Agosti 10, 2020 Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

# SERIKALI YAZISHUKURU UFARANSA, NORWAY KUCHANGIA MIRADI YA UMEME VIJIJINI



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier (kulia) pamoja na Ujumbe kutoka Ubalozi wa Norway hapa nchini. Kikao hicho kilichojadili masuala ya ushirikiano katika sekta ya nishati, kilifanyika Agosti 27, 2020 Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam.

**Veronica Simba –  
Dar es Salaam**

**S**erikali ya Tanzania imezishukuru nchi za Ufaransa na Norway kwa mchango wake mkubwa walioutoa na wanaoendelea kuutoa katika kuwezesha utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani alitoa shukrani hizo jijini Dar es Salaam, Agosti 27, 2020 wakati wa kikao baina yake na Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Frederic Clavier pamoja na Bjorn Midthun, ambaye ni Afisa Mwandamizi kutoka Ubalozi wa Norway nchini Tanzania.

"Mmefanya kazi nzuri sana katika kutuwezesha

kutekeleza miradi ya umeme vijijini. Ushirikiano wenu umetuwezesha kufikia hatua hii tuliyopo leo. Kwa niaba ya Serikali, ninawashukuru sana," alisitiza Waziri.

Akidadavua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, Dkt Kalemani alisema hadi sasa zaidi ya vijiji 9,512 ambavyo ni zaidi ya asilimia 85 ya vijiji vyote 12,268 vilivyopo nchini, vimeshafikiwa na umeme.

Aidha, alueleza Ujumbe huo kutoka Ufaransa na Norway kuwa vitongoji takribani 25,000 vimekwishafikiwa umeme kati ya 64,339 vilivyopo nchini hivyo ameziomba nchi hizo kuendelea kutoa mchangwo katika kuwezesha kutekeleza kazi iliyobaki ya kupeleka umeme kwa vijiji na vitongoji vilivyosalia nchini.

Alisema umeme ni injini ya uchumi huku akipambanua kuwa pasipo

**INAENDELEA UK.**

**36**



Ujumbe kutoka Balozi za Ufaransa na Norway nchini Tanzania, wakiwa katika kikao na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake (hawako pichani). Kikao hicho kilichojadili masuala ya ushirikiano katika sekta ya nishati, kilifanyika Agosti 27, 2020 Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam.

# SERIKALI YAZISHUKURU UFARANSA, NORWAY KUCHANGIA MIRADI YA UMEME VIJIJINI

(REA) Mhandisi Amos Maganga na baadhi ya Maafisa Waandamizi kutoka REA, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Balozi za Norway na Ufaransa hapa nchini.



Baadhi ya Viongozi na Wataalamu kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakiwa katika kikao cha Waziri mwenye dhamana, Dkt Medard Kalemani na Ujumbe kutoka Balozi za Ufaransa na Norway nchini Tanzania (hawako pichani). Kikao hicho kilichojadili masuala ya ushirikiano katika sekta ya nishati, kilifanyika Agosti 27, 2020 Ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam.

**INATOKA UK.**

**35**

umeme wa uhakika, haiwezekani kwa nchi yoyote kuwa na maendeleo ya kiuchumi.

Aliongeza kuwa jitihada za makusudi zinazoendelea kufanya na Serikali hususani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme, pamoja na mambo mengine, ndizo zimeiwesha Tanzania, kuingia katika uchumi wa kati.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika kikao hicho, Balozi Clavier pamoja na Bwana Midthun, walimhakikishia Waziri Kalemani kuwa Serikali

za nchi zao zitaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuwezesha miradi mbalimbali ya umeme.

Pamoja na kueleza utayari wa kuendelea kuisaidia Tanzania, Viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kuzingatia viwango vya ubora katika kutekeleza miradi husika ambapo Waziri Kalemani amewahakikishia kuwa, ubora na uaminifu ni masuala yanayopewa umuhimu wa hali ya juu.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Styden Rwebangira, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier (kushoto) na Bjorn Midthun, ambaye ni Afisa Mwandamizi kutoka Ubalozi wa Norway hapa nchini. Waziri alifanya kikao na Ujumbe husika, Agosti 27, 2020 Ofisi ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam, kujadili masuala ya ushirikiano katika sekta ya nishati.

# JARIDA HILI LA MTANDAO NI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**

Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018  
Nukushi +255-26-2320148

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)